

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)



TAARIFA KWA UMMA

UPATIKANAJI WA HATI MILIKI YA ARDHI YA MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (LIQUEFIED NATURAL GAS - LNG) ENEO LA LINDI

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linatoa taarifa kwa umma juu ya upatikanaji wa hati miliki ya ardhi kwa ajili ya mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG). Upatikanaji wa hati miliki hii ni muendelezo wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Kamishna wa Ardhi juu ya ubatilishaji wa miliki za ardhi ya tarehe 30 Oktoba 2015 na kuchapishwa katika gazeti la Daily News la tarehe 17 Novemba 2015.

Eneo la ardhi hii lipo katika kiwanja Na.1-Kitalu "A", Likong'o katika Manispaa ya Lindi na lilipendekezwa na kuchaguliwa kwa pamoja kati ya TPDC na wawekezaji kutoka kampuni za kimataifa za utafutaji mafuta na gesi asilia (IOCs) zinazofanya kazi zake hapa nchini. Kupatikana kwa hati miliki ya ardhi hii ni hatua muhimu katika utekelezaji wa mradi huu ambao unalenga kuendeleza gesi asilia iliyogunduliwa katika kina kirefu cha bahari ya Hindi upande wa Tanzania. Mradi huu utakapokamilika utawezesha uzalishaji wa gesi asilia kwa mahitaji ya ndani ya nchi, kiasi kingine kitasafirishwa nje ya nchi na kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Ardhi ambayo itatumika kujenga mradi huu ni hekta 2,071.705 na inamilikiwa na TPDC. Sambamba na mradi wa "LNG" lipo eneo lipatalo zaidi ya hekta 17,000 linalozunguka mradi. Eneo hili litatumika kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa vya kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na gesi asilia.

Serikali kupitia TPDC inatoa wito kwa wananchi kujiepusha na ununuzi wa maeneo haya kwani tayari yamekwisha tengwa kwa miradi yenye manufaa kwa Taifa na hivyo kujigawia au kuvamia itakuwa ni kinyume cha sheria za nchi.

**Imetolewa na;
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania,
P.O.Box 2774,
Dar-es-Salaam.
Tanzania.**